**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA SERIKALI YA KAMULI

**Juni, 2024**

**KAMULI SEC -KYERWA DC**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0787 681605/0767 681605**

**Makamu Mkuu wa Shule 0762652847/0683780384**

**Matron 0624334624**

**Shule ya Sekondari Kamuli**

**S.L.P. 64 ,KYERWA**


**Tarehe 14/06/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAMULI HALMASHAURI YA KYERWA MKOA KAGERA MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024. na atasoma tahasusi ya HGL

Shule ya Sekondari KAMULI ipo umbali wa Kilometa 35 Kaskazini//Magharibi mwa Mji wa NKWENDA.Usafiri wa basi kutoka mjini NKWENDA unapatikana katika kituo cha mabasi NKWENDA Nauli ni Shilingi 4,000/= na 15,000/= kwa pikipiki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13 Agosti,2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13 Agosti,2024.Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31 Agosti,2024.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Sketi mbili za rangi ya pinki zenye rinda box mbili mbele na nyuma na ndefu karibu na kifundo(kisigino) cha mguu kwa Wasichana.
ii. Mashati mawili meupe tetroni ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama(Waislamu tu).
iv. Sare ya Michezo ni raba nyeupe na tracksuit ya rangi ya njano moja aina ya sport Kwa wasichana.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili ndefu nyeupe za shule;
vii. Sweta moja ya rangi blue.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni gauni moja ya rangi ya zambarau kitambaa kigumu.
ix. Na aje na tai moja ya rangi ya pink ndefu.
x. Tisheti (T-shirt) moja ya rangi ya njano yenye kola.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 10 aina ya counter book quire 2. Na mathematical set.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka.Moja kila muhula
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika yaani HISTORY,GEOGRAPHY & KIINGEREZA.Eg.physical geography,human and economic geography,practical geography,kamusi ya kiingereza (oxford advanced learners

dictionary).Kwa kiingereza PLAYS The lion and the jewel by Soyinka,W.,The trials of brother Jero by Soyinka,W.,The dilemma of the Ghost by Aidoo,A.A.,The government Inspector by Gogol,N.,Literature analysisi,.and NOVELS A walk in the night and other stories houseboy by Guma,A.,The old man and the medal by Oyono,F.,The concubine by Amadi,E.,POEMS selected poems by TIE ,Growing up with poetry by Rubadiri,D.,General studies book.history advanced learner f5&6 book 1&2.

iv. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya futi 2½x 6 .
v. Mashuka Jozi 2 rangi pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 kubwa zenye mifuniko na beseni moja.
ix. Siko 1, jembe 1, reki 1, mifagio hardbrooms 1,rubber squizer 1 panga 1,mifagio ya chepeo miwili. 1.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango hii inaweza kutumwa kupitia akaunti ya shule NMB 31901100057 yenye jina KAMULI SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT.Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi nyuma ya pay slip na uje nayo shuleni unaporipoti.**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutokuonekana kwenye nyumba za walimu bila kibali.
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na shule.Mawasiliano yote yafanyike kupitia simu ya mkuu wa shule tu.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).RUHUSA ZOTE ZITATOLEWA NA MKUU WA SHULE TU.

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
    i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
    ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
    iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
    iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
    v. Bima ya afya ya mwanafunzi ni lazima au sh.50,400/=kwa mwaka .
5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule EMMANUEL KAIZA MUTIGANZI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0787 681 605/ 0767 681 605. 0624334624.**

## OFISI YA RAIS TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA

## SHULE YA SEKONDARI KAMULI

## S.L.P 64 KYERWA.

### FOMU YA TAARIFA ZA MWANAFUNZI

**1.TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI.**

i. Jina la mwanafunzi ……………………………………………….jinsi………Tarehe ya kuzaliwa...........................
ii. Shule ya Sekondari aliyotoka ……………………………………………………………………………………………….
iii. Jina la baba…………………………………………….kazi yake………………………….Simu…………………………….
iv. Jina la mama ……………………………………………kazi yake………………………….Simu…………………………
v. Kijiji/mtaa wanapoishi…………………………………..Wilaya ……………………………Mkoa……………………….
vi. Dini………………………………………………………………………………………………………………………………
vii. Majina ya ndugu wa karibu wa mawanafunzi .;
a………………………………………………………………………anakoishi…………………………..simu…………………….
b……………………………………………………………………..anakoishi………………………..simu……………………..
c……………………………………………………………………..anakoishi………………………..simu……………………..

**2.KUKUBALI NA KUTII SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE.**

Mimi (Jina la mwanafunzi)………………………………………………………naahidi sitashiriki kabisa katika fujo /migomo na kutenda makosa ya jinai shuleni na maeneo mengine .Pia naahidi kuzifuata sheria na taratibu zote za shule kwa faida yangu binafsi ,kwa shule na kwa Taifa kwa ujumla .Endapo nitakwenda kinyume na taratibu,kanuni na sheria za shule nakubali kufukuzwa shule au ksimamishwa masomo na kupewa adhabu nyingine kulingana na sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na sheria ya makosa ya jinai ya mwaka 2002.

**JINA LA MWANAFUNZI……………………………………………… SAINI…………………………………………TAREHE……………**

**JINA LA MZAZI……………………………………………………….SAINI………………………………………..TAREHE……………**

**OFISI YA RAIS TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

**SHULE YA SEKONDARI KAMULI**

**S.L.P. 64**

**KYERWA.**

**…………………………………………..**

**FOMU YA KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI**

**MGANGA MKUU/MGANGA MFAWIDHI**

**KITUO CHA AFYA/ HOSPITALI**

**………………………………………………**

**……………………………………………..**

**……………………………………………..**

**YAH:KUPIMA AFYA YA MWANAFUNZI ……………………………………………………………….KWA AJILI YA KUJIUNGA NA SHULE.**

Kijana huyu amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii Kamuli Sekondari ,hivyo naomba uthibitishe hali ya afya yake kabla ya kuanza masomo yake hapa shuleni kwa haya yafuatayo;

**1.TB……………………………………………………………………………………………………………………………………**
**2.HB…………………………………………………………………,,,………………………………………………………………**
**3.STOOL………………………………………………………………………………………………………………………………**
**4.URINE………………………………………………………………………………………………………………………………**
**5.EYE/EARS…………………………………………………………………………………………………………………………..**
**6.ATHMA……………………………………………………………………………………………………………………………..**
**7.TYPHOID……………………………………………………………………………………………………………………………**
**8.OTHERS………………………………………………………………………………………………………………………..……**
**Maoni ya Daktari /mganga mfawidhi**……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………………………………….

**JINA LA DAKTARI/MGANGA MFAWIDHI………………………………………………SAINI……………………………MHURI…………………………………..**